# Mchango wa Tafsiri za J.K. Nyerere katika Maendeleo ya Fasihi ya Kiswahili

*Hadija Jilala*
*Chuo Kikuu Huria cha Tanzania*

**Ikisiri**

**Makala hii inatathmini mchango wa tafsiri za J.K. Nyerere katika maendeleo ya fasihi ya Kiswahili ili kuona ni kwa kiasi gani kazi zake za tafsiri zimeweza kukuza na kuendeleza fasihi ya Kiswahili. Kwa maneno mengine, makala hii inaonesha jinsi kazi za tafsiri za J.K Nyerere zilivyochangia maendeleo ya fasihi ya Kiswahili. Ili kufikia lengo hilo, makala hii inatumia data kutoka katika vitabu viwili vya tafsiri ambavyo ni *Julius Kaizari* (1963) na *Mabepari wa Venisi* (1969) vya mwandishi Shakespeare vilivyotafsiriwa kutoka lugha ya Kiingereza kwenda Kiswahili. Data za makala hii zimekusanywa kwa kutumia mbinu ya usomaji makini. Uchambuzi, uwasilishaji wa data na mjadala wa matokeo ya uchunguzi umeongozwa na Nadharia ya Skopos ya Hans J. Vermeer (1970). Matokeo ya uchunguzi yanaonesha kuwa kazi za tafsiri zimetoa mchango mkubwa katika maendeleo ya fasihi ya Kiswahili kifani na kimaudhui. Kwa sababu kazi hizo zimeitajirisha fasihi ya Kiswahili, kuibua msamiati, mbinu za kisanaa, mtindo, misemo, kuchagiza utunzi wa tamthiliya na maendeleo ya dhamira katika fasihi ya Kiswahili. Kwa ujumla, tunaweza kusema kuwa kazi za tafsiri za J.K. Nyerere zimechangia kwa kiasi kikubwa kukuza na kuendeleza fasihi ya Kiswahili sio tu nchini Tanzania bali duniani kote.**

**Maneno Muhimu**: *Tafsiri, Tafsiri ya Kifashi, Maendeleo, Fani, Maudhui*

**Utangulizi**

Dhana ya tafsiri kama zoezi la uhawilishaji wa mawazo na ujumbe kutoka katika lugha moja kwenda lugha nyingine, imefasiliwa na kujadiliwa na wataalamu mbalimbali. Miongoni mwa wataalamu hao ni Catford (1965), Nida (1964), Nida na Taber (1969), Newmark (1988), na Mwansoko (1996). Akifasili dhana ya tafsiri, Catford (1965) anaeleza kuwa tafsiri ni zoezi la kuchukua mawazo yaliyo katika maandishi kutoka lugha moja (lugha chanzi) na kuweka badala yake mawazo yanayolingana na hayo katika lugha nyingine (lugha lengwa). Aidha, Mwansoko (1996) anafasili tafsiri kama zoezi la uhawilishaji wa mawazo ama ujumbe ulio katika maandishi kutoka lugha chanzi kwenda katika lugha lengwa. Pia, Nida na Taber (1969) wanaeleza kuwa tafsiri hujumuisha kuzalisha upya ujumbe wa lugha chanzi kwa kutumia visawe vya asili vya lugha lengwa vinavyokaribiana zaidi na lugha chanzi kimaana na kimtindo.

Kwa ujumla, wataalamu hawa wanatilia mkazo uzalishaji mpya wa ujumbe kwa kutumia visawe asili vinavyokaribiana na matini chanzi kimaana na kimtindo. Kutokana na fasili hizo tunaona kuwa tafsiri hufanywa kwa kuhamisha ujumbe uliopo katika maandishi, ni zoezi la uhawilishaji wa mawazo au ujumbe unaotafsiriwa nakuwa na visawe vinavyokaribiana katika lugha lengwa. Visawe hivyo vinaweza kuwa sawa kutokana na sababu za utofauti wa kiisimu, kihistoria, kiutamaduni na mazingira. Kwa ujumla, tafsiri ni mchakato wa uhawilishaji wa mawazo, ujumbe au maana katika maandishi kutoka lugha moja kwenda nyingine (kutoka lugha chanzi kwenda lugha lengwa).

Kwa hiyo, kupitia fasili za wataalamu mbalimbali ambazo zimetolewa kuhusu tafsiri tunaweza kuhitimisha kuwa, tafsiri ni mchakato ambao huhusisha lugha chanzi, lugha lengwa, matini, mfasiri mwenye weledi, zana za kufasiria, kanuni, taratibu, na tamaduni. Katika muktadha huo, tafsiri ni suluhisho la mawasiliano ambapo husaidia kueleweka kwa maana na ujumbe uliokusudiwa katika matini chanzi kwa hadhira lengwa. Hivyo, tunaweza kusema kuwa tafsiri ni taaluma ya uhawilishaji wa mawazo katika maandishi kutoka lugha chanzi kwenda lugha lengwa kwa kuzingatia isimu, muktadha na utamaduni. Hii ni kwa sababu tafsiri huweza kuunganisha jamii zinazozungumza lugha mbili tofauti na kufanya jamii hizo ziweze kusikilizana na kuelewana. Aidha, kufahamu mila, desturi,

tamaduni na kaida za jamii nyingine. Vile vile, tafsiri husaidia kufahamu maudhui yaliyokusudiwa katika matini chanzi ili yaweze kuifikia hadhira lengwa.

Katika kufafanua dhima za tafsiri, Mwansoko (2016) anaeleza kuwa tafsiri ina manufaa makubwa sana kwa binadamu. Kwa sababu tafsiri inawezesha mawasiliano baina ya watu wenye lugha zinazotofautiana, ni nyenzo ya kueneza utamaduni kutoka jamii moja hadi nyingine na ni mojawapo ya mbinu muhimu za kujifunza lugha za kigeni. Aidha, tafsiri ina dhima ya kukuza na kueneza lugha hasa kupitia ule mchakato wa kuhamishia miundo ya misemo ya lugha chanzi kwenye lugha lengwa. Pia, tafsiri ni liwazo kwa mfasiri anapofanikiwa kukamilisha kazi yake kwa ufanisi (Mwansoko, 1996). Hivyo, kutokana na dhima hizi ni dhahiri kuwa mfasiri anapaswa kuhakikisha tafsiri yake inakidhi dhima hizi.

Tukiangalia kwa haraka haraka, tutaona kuwa tafsiri ni eneo ambalo limekuwa likishughulikiwa katika nyanja na maeneo mbalimbali ya maisha ya binadamu. Aidha, tafsiri ni taaluma ambayo inafungamana na maisha ya binadamu kwa sababu siku zote na katika mazingira yote mwanadamu hawezi kuepuka tafsiri. Hii ni kwa sababu wanadamu wanaishi ulimwengu tofauti ambapo wanaishi katika mazingira, muktadha na utamaduni wa lugha tofauti. Hivyo, tafsiri inafanya kazi ya kuunganisha jamii na kufanya watu waweze kuhusiana, kuwasiliana na kufahamiana. Kwa mantiki hiyo, ni dhahiri kuwa bila tafsiri dunia ingekuwa gizani kuhusu jamii moja na jamii nyingine, upatikanaji na uelewa wa maarifa ungekuwa finyu kwa sababu hakuna jamii ambayo ingeelewa maarifa yaliyogunduliwa na kubuniwa na jamii nyingine.

**Tafsiri za Kifasihi**

Hassan (2011: 4) anaeleza kuwa, tafsiri ya fasihi ni tafsiri ambayo hutofautiana na tafsiri nyingine kwa kuwa ni lazima iakisi picha, mawazo na ubunifu wa mwandishi. Anaendelea kueleza kuwa, tafsiri ya fasihi haina budi kuakisi masuala yote ya kifasihi yanayojitokeza katika matini chanzi kama vile, sauti, uteuzi wa maneno na lugha ya picha. Kutokana na masuala hayo, tafsiri katika fasihi imekuwa ikichukuliwa kama eneo lenye changamoto nyingi za kiufundi. Katika muktadha huo, wanazuoni na watafiti wa tafsiri wanadai kuwa ni vigumu sana kutafsiri matini za kifasihi (Newmark, 1988; Mwansoko, 1996; Nida, 2005).

Hivyo, tafsiri ya fasihi hufanywa kwa lengo la kuhawilisha mawazo na ujumbe wa matini chanzi ya kifasihi kutoka lugha moja ambayo ni lugha chanzi kwenda lugha nyingine. Katika kufasili tafsiri ya ushairi, Bazzuro (2008) anaeleza kuwa, tafsiri ya fasihi ni ile inayohusisha ufasiri wa matini za ushairi, tamthiliya, riwaya na kazi za kifasihi zilizoandikwa, nyimbo, mashairi, makala za kifasihi na hadithi fupi. Kwa uapande mwingine, Wechsler (1998: 4) anafafanua kwamba, tafsiri ya fasihi ni sanaa isiyo ya kawaida. Sanaa hii inamhusisha mtu kuketi kwenye meza, kuandika fasiri kwa kazi isiyo yake, ambayo ina jina la mtu mwingine. Kwa hiyo kazi ya mfasiri hutokea kama uigaji tu au isiyo na uasili. Mfasiri huchukua mawazo ya msanii, huyajengea picha kwa kuyaandika katika lugha nyingine.

Mambo ya msingi na ya kuzingatiwa katika kutafsiri fasihi ni kwamba mfasiri hana budi kuwa na ujuzi wa fasihi, hususani mbinu mbalimbali za kisanaa. Mfasiri lazima ajue sarufi na utamaduni wa lugha anazozifanyia kazi. Katika eneo la fasihi, kumekuwepo na raghba kubwa miongoni mwa wanazuoni wa Tanzania kufasiri riwaya, tamthiliya na mashairi kutoka lugha ya Kiingereza na wakati mwingine lugha nyinginezo za kimataifa. Hata hivyo, si wote wanaofanya kazi hizi za kufasiri ni wafasiri weledi. Mwansoko (2016) anasema, kwa upande wa wafasiri wa fasihi, si kwamba tu wengi wao hawana taaluma ya tafsiri ambayo ingewajuvya misingi muhimu ya kuifanya kazi hiyo kwa ufanisi, lakini pia baadhi yao si wanafasihi. Wameifanya kazi ya kutafsiri fasihi kwa mapenzi tu, aghalabu kama shughuli ya ziada ya kuburudisha nafsi na isiyo ya kulipwa ujira (Waingereza huiita shughuli ya namna hii '*hobby*').

Katika utangulizi wa tafsiri ya *Juliasi Kaizari* (1963), Mwalimu Nyerere, kwa mfano, amekiri: 'Nia yangu ilikuwa kupata jambo la kufanya wakati kazi zangu za kawaida zilipokuwa zimenichosha sana na nataka kiburudisho.' Lakini, kwa bahati Nyerere alikuwa akifundisha somo la Kiswahili

katika shule za sekondari wakati wa ukoloni. Hivyo, ni mfasiri mwanafasihi (Mwansoko, 2016). Taaluma ya tafsiri inaelekeza kwamba, mfasiri bora wa fasihi ni mwanafasihi ambaye pia ana misingi ya kisayansi ya kutafsiri. Ama kuhusu tafsiri katika medani ya taaluma za Kiswahili, kwa kiwango kikubwa hapa kuna uzingativu wa misingi na kanuni za tafsiri kwa vile ndipo panapotolewa mafunzo ya taaluma ya tafsiri.

Hata hivyo, tafiti zinaonesha utanzu wa tamthiliya ndiyo utanzu uliotafsiriwa zaidi kuliko tanzu nyingine za fasihi. Mwansoko (2006) anaeleza kuwa tamthiliya ni utanzu uliotafsiriwa sana kutokana na malengo makuu mawili; lengo la kuigizwa na lengo la kusomwa. Pia, umefasiriwa sana kutokana na kwamba, ulikuwa ni utanzu mpya katika Afrika, hivyo wageni na wenyeji walitafsiri kwa lengo la kuutambulisha katika mazingira ya Kiafrika. Vilevile, umeonekana kutafsiriwa sana kutokana na urahisi wa lugha yake, kwani tamthiliya hutumia maneno machache na yanayoeleweka bila hata ya ufafanuzi wa kina kama ilivyo katika riwaya. Zaidi ya yote, umefasiriwa sana kutokana na umuhimu wa maudhui yake ambayo hujibainisha katika masuala mtambuko duniani kote.

Method (2015) anasema, kazi za tafsiri zina mchango mkubwa sana katika ukuaji wa fasihi ya Kiswahili, tamthiliya ikiwemo. Fasihi ya Kiingereza inaonekana kunufaika sana kutokana na tafsiri ya fasihi za Kiyunani, Kiroma, Kirusi na Kifaransa (Wafula 1999). Ryanga (1985) anaeleza kuwa tafsiri ina dhima kimaudhui na kifani katika fasihi ya Kiswahili na fasihi nyinginezo. Kimaudhui, anabainisha kuwa aina mpya ya maudhui huweza kuibuka katika fasihi lengwa. Kifani, anazitaja faida za kazi za tafsiri katika fasihi ya Kiswahili kuwa ni pamoja na kuibuka kwa mitindo mipya ya uandishi na kuingia kwa tanzu mpya katika fasihi ya Kiswahili.

Aidha, watafiti na wataalamu wengine wa tafsiri wanadai kuwa matini za kifasihi ni ngumu kufasirika. Matini hizo hushindiliwa dhana nyingi za kitamaduni. Kwa hiyo, mfasiri anayeamua kufasiri kazi ya kifasihi ni lazima azifahamu vema tamaduni za jamii inayotumia lugha chanzi (LC) na jamii inayotumia (LL) na aweze kuziwianisha tamaduni hizo ipasavyo. Bila kuwepo na uwiano wa kitamaduni, tafsiri haitawasilisha maana inayotakiwa na hivyo mawasiliano hayatakuwepo (Newmark, 1988 na Mwansoko na wenzake, 2006).

Mpaka sasa tumeshuhudia tafsiri ya matini za kifasihi ambazo zinafanywa kutoka lugha mbalimbali duniani ikiwemo Kiingereza, Kijerumani, Kijapani, na Kichina, hizi zikiwa ni baadhi tu ya lugha hizo. Baada ya ujio wa wageni ambao ni Waarabu na wakoloni Wajerumani na Waingereza walioingia nchini kazi nyingi za fasihi zilifanyika. Tafsiri zilizofanyika ni pamoja na kutafsiri vitabu vya fasihi zao, kutafsiri vitabu vya dini kama vile Kuran na Biblia. Wazawa nao walifanya kazi za kutafsiri matini za lugha za kikabilia kwenda Kiingereza na Kiswahili pia. Moja ya mfasiri maarufu aliyetafsiri kazi za fasihi ya Kiingereza kwenda Kiswahili ni Mwalimu J.K. Nyerere ambaye alitafsiri matini za tamthiliya zilizotungwa na kuandikwa na William Shakespeare ambazo ni *Julius Kaizari* (1963) na *Mabepari wa Venus* (1969).

**Muhtasari Kuhusu Mfasiri J.K. Nyerere**

Mwalimu J.K. Nyerere alikuwa Rais wa kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ndiye aliyekuwa mwasisi wa taifa la Tanzania. Nyerere anatambulika kama baba wa taifa la Tanzania kutokana na heshima alizojizolea kitaifa na kimataifa katika kuiongoza nchi ya Tanzania tangu harakati za kudai uhuru, kupata uhuru na kuwa taifa huru linalojitegemea. Aliiongoza Tanzania kwa kipindi kirefu kuanzia mwaka 1961 mpaka alipong'atuka mwaka 1985 Mwalimu J.K. Nyerere alikuwa ni muumini wa falsafa na itikadi ya siasa ya ujamaa na kujitegemea na muasisi wa Azimo la Arusha lililofanya Tanzania kuwa ni nchi ya Ujamaa na kujitegemea. Miongoni mwa kazi alizozifanya ni pamoja na kuandika vitabu mbalimbali kama vile *Uhuru na Kazi, Inawezekana Timiza Wajibu Wako, Linalowezekana leo Lisingoje Kesho* na *Kupanga ni Kuchagua.* Lakini pia alifanya kazi ya kutafsiri matini za kifasihi ambapo alitafsiri kazi za tamthiliya zilizoandikwa na William Shakespeare za Julius Kaizari (1963) na *Mabepari wa Venisi* (1969). Hata hivyo, si lengo la makala hii kujadili kuhusu Mwalimu Nyerere ama kutoa historia yake bali lengo ni kutathmini mchango wa tafsiri alizozifanya katika maendeleo ya fasihi ya Kiswahili. Hivyo, tuliona kuwa kutafsiri vitabu viwili ni mchango mkubwa si katika lugha tu bali katika fasihi ya Kiswahili. Kwa kuzingatia hilo

tuliona kuna haja ya kufanya thathmini ya mchango wa tafsiri zake katika maendeleo ya fasihi ya Kiswahili. Kwa kufanya hivi tutaweza kuonesha mchango ambao J. K. Nyerere ameutoa katika maendeleo ya fasihi ya Kiswahili.

**Historia ya Tafsiri ya Fasihi**

Hapa Afrika, tafsiri ya matini za kifasihi ina historia ndefu. Kazi hii imefanyika tangu kipindi cha ujio wa wageni ambao ni wakaloni waliongia katika nchi za Afrika hususan nchi za Afrika Mashariki. Katika kipindi hicho, tafsiri ya matini za kifasihi ilifanyika kwa lengo la kueneza utamaduni wa nchi za Ulaya na Asia. Aidha, tafsiri ililenga kutoa mafunzo kuhusu lugha, tamaduni, dini na ustaarabu wa nchi tawala kwa wenyeji. Baadhi ya kazi za fasihi zilitafsiriwa katika kipindi hicho na kazi za tamthiliya ndizo zilitafsiriwa kwa wingi zaidi. Kwa mfano, katika kuelezea tafsiri ya kazi za tamthiliya Wafula (1999) anaeleza kuwa kuna aina nne za tamthiliya zilizotafsiriwa. Kwanza, kuna tamthiliya zilizotafsiriwa kutoka lugha nyingine hadi Kiingereza na kisha kutafsiriwa kwa Kiswahili, mfano wa tamthiiya hizo ni pamoja na *"Mchuuzi Muungwana"* ya Morrison (1961), nyingine ni "*Mfalme Edipode"* ya Mushi (1973) na ile ya "*Mkaguzi Mkuu wa Serikali"* ya Nikolai Gogol (1979). Pia, kuna tamthiliya zilizoandikwa kwa Kiingereza na wageni na kutafsiriwa kwa Kiswahili mfano wa tamthiliya ilizotafsiriwa katika mfumo huu ni pamoja na tamthiliya zote za Shakespeare za *Julius Kaizari* (1963) na *Mabepari wa Venisi* (1969). Vilevile, kuna tamthiliya zilizoandikwa kwa Kiingereza na Waafrika kisha zikatafsiriwa kwa Kiswahili mfano wa tamthiliya hizo ni "*Maswaibu ya Ndugu Jero"* ya Soyika (1975) *na "Mzalendo Kimathi"* ya Ngugi wa Thiongó (1978) ni mifano ya tamthiliya za aina hii. Kuna tamthiliya zilizoandikwa katika lugha nyingine za Kiafrika na kutafsiriwa katika Kiswahili mfano wa tamthiliya hizo ni "*Nitaolewa Nikipenda"* ya Ngugi wa Thiongó (1981).

Pia, tafsiri huweza kusababisha kuingia kwa tanzu mpya katika fasihi lengwa. Kama inavyobainishwa na wataalamu mbalimbali, tanzu za fasihi hutofautiana kutoka jamii moja kwenda nyingine (Samwel 2012, Samwel na wenzake 2013). Hivyo kazi fulani ya fasihi inapotafsiriwa kutoka katika jamii moja kwenda nyingine ambayo haina utanzu husika, jamii lengwa hunufaika kwa kuweza kupata aina mpya ya utanzu. Fasihi ya Kiswahili, kwa mfano, imenufaishwa sana na utanzu wa tanzia ambao umeingizwa katika fasihi hiyo kutokana na kazi za tafsiri za kifasihi kama vile *Oedipus the King* (Sophocle*s*) ambayo imetafsiriwa Kiswahili, *Mfalme Edipode* (S. Mushi), Tafsiri katika fasihi ni eneo lenye historia ndefu ambalo limeshughulikiwa kwa muda mrefu. Ongezeko hili limechangia kuwepo kwa kazi nyingi za fasihi ya Kiswahili kama vile tamthiliya, riwaya, hadithi fupi, mashairi na hata tungo nyingine ambazo zimetafsiriwa kutoka lugha za kigeni na za Kiafrika kwenda katika lugha ya Kiswahili, na hatimaye kufanya kazi hizo kusomwa kwa lugha ya Kiswahili. Vitabu vingi vya lugha ya kigeni hasa ya Kiingereza vimetafsiriwa kwa Kiswahili na hivyo kuifanya fasihi ya Kiswahili ipige hatua kubwa ya kimaendeleo. Baadhi ya kazi hizi ni kama vile: The Well of Gining - *Kisima cha Giningi* cha Muhamed Said (1968), Maisha Yangu *Moya Zhizn*, riwaya ya Andrei Zhukov 1968 Kiswahili-Kirusi, I will marry when I want - *Nitaolewa Nikipenda*, The Beautiful Ones are Not yet Born - *Wema Hawajazaliwa*, The Taste of Heaven - *Aliyeonja Pepo* Tamthiliya, The Government Inspector -*Mkaguzi Mkuu wa Serikali* Tamthiliya Christon Mwakasaka 1979 Kiingereza-Kiswahili, Anthology of Swahili Poetry - *Kusanyiko la Mashairi*, The Black Hermit - *Mtawa Mweusi*, Song of Lawino - *Wimbo wa Lawino*. Katika miaka ya 1930 kazi za fasihi za kigeni zilizotafsiriwa kwa Kiswahili zilikuwa chache mno. Kazi hizo zilitokana na lugha za mataifa ya Ulaya na Asia. Baada ya Uhuru kupatikana katika miaka ya 1960 hadi sasa tumeshuhudia kazi nyingi za fasihi ambazo zimetafsiriwa kutoka lugha ya Kiswahili kwenda lugha ya Kiingereza na pia kutoka lugha za kikabila kwenda katika lugha ya Kiswahili. Baadhi ya kazi zilizotafsiriwa ni: Oedipus The King *Mfalme Edipode* (Sophocles), Antigone *Antigoni* (Sophocles), Merchant of Venice *Mabepari wa Venisi* (W. Shakespeare), The Government Inspector *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* (N. Gogol) na Animal Farm *Shamba la Wanyama* (G. Orwell). Zipo tamthiliya mbalimbali zilizofasiriwa kutoka katika lugha ya Kiingereza kwenda lugha ya Kiswahili, baadhi yake ni *Mabepari wa Venisi* (1969), *Juliasi Kaizari* (1969), *Tufani* (1969), *Mtawa Mweusi* (1970)*, Mkaguzi Mkuu wa Serikali* (1979) na *Nitaolewa Nikipenda* (1982).

**Mkabala wa Kinadharia**

Uchambuzi, uwasilishaji wa data na mjadala wa makala hii umeongozwa na Nadharia ya Skopos. Nadharia ya *Skopos* iliyoasisiwa na Hans J. Vermeer katika miaka ya 1970 huko Ujerumani. Hii ni miongoni mwa nadharia za uamilifu ambazo ziliibuka miaka ya 1970 na 1980. Kipindi ambacho nadharia za isimu kama kiunzi cha kuchunguza, kuchambua na kushughulikia tafsiri zilipingwa na baadhi ya wataalamu na wanazuoni wa tafsiri na hatimaye kuonekana ni nadharia ambazo zinashindwa kufumbata na kukabili masuala ya tafsiri.

Kwa sababu hiyo, nadharia za kidhima ama kiuamilifu zilianzishwa kwa lengo la kupinga nadharia za isimu katika tafsiri. Lengo la nadharia hizi lilikuwa ni kuipuuza matini chanzi na kuweka mkazo katika lengo na hadhira lengwa huku msisitizo ukiwa katika uamilifu wa matini. Wanauamilifu walitilia mkazo katika nafasi na kazi ya mfasiri kama muumbaji wa matini lengwa na kuweka kipaumbele kwenye lengo la kuzalisha matini lengwa. Kwa hiyo, nadharia za uamilifu ni nadharia zilizojikita katika uhawilishaji na kuitazama tafsiri kutoka kwenye ulinganifu wa kiisimu kwenda kwenye ubora wa kiuamilifu au kidhima. Tafsiri inachukuliwa kuwa ni mchakato wa mawasiliano ya muingiliano wa tamaduni ambao matokeo au zao lake ni matini yenye uwezo wa kufanya kazi kwa ufanisi katika mazingira na muktadha mahususi wa matumizi (Schaffner, 1998a: 3). Miongoni mwa nadharia za uamilifu zilizoibuka kwa lengo hilo ni Nadharia ya Aina za Matini, Nadharia ya Utangamani, Nadharia ya Uamuzi wa Mfasiri, Nadharia ya *Skopos* na Nadharia ya Uchambuzi Matini. Sehemu hii itajikita katika kuhakiki Nadharia ya *Skopos* katika tafsiri. Lengo ni kuhakiki matumizi ya mihimili ya mawazo ya nadharia ya *Skopos* katika kutafsiri matini za kiutamaduni kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza ili kuibua ubora na upungufu wake katika kutafsiri na hatimaye kutoa mapendekezo.

Neno 'Skopos' chimbuko lake ni lugha ya Kigiriki, neno hili hutumika kama msamiati wa kiufundi unaorejelea lengo la tafsiri. Kulingana na Wananadharia ya *Skopos*, kanuni ya msingi inayoukilia lengo la tafsiri ni lengo au Skopos ya kitendo cha kutafsiri. Msingi wa Nadharia ya *Skopos* ni kuiona tafsiri kama utekelezaji wa kitendo cha tafsiri kwa kuzingatia matini asilia. Ni nadharia iliyoleta mageuzi ya mtazamo uliokuwepo wa kuiona tafsiri kama kitendo cha kiisimu na hivyo kuitazama nadharia ya tafsiri kama dhana ya uamilifu na utamaduni wa jamii. Uhawilishaji huu wa mtazamo wa tafsiri ulitokana na hamasa ya Nadharia ya Mawasiliano, Vitendo, Isimu, Matini, Nadharia ya Matini na pia kutoka katika mikabala ya kifasihi kwenda kwenye nadharia za upokezi (Iser, 1978).

Nadharia ya *Skopos* inashughulikia kwa undani mambo yaliyosisitizwa na kutiliwa mkazo katika Nadharia ya Vitendo. Mambo hayo ndiyo yamesaidia katika tafsiri ya matini zisizokuwa za kifasihi, tafsiri ya makala za kisayansi na kitaaluma, maelekezo ya matumizi, mwongozo wa utalii na mikataba. Katika nadharia hii, msisitizo upo katika uzingativu wa muktadha unaoizunguka tafsiri, kwamba muktadha hautakiwi kupuuzwa. Muktadha huhusisha mambo kama vile utamaduni, hadhira, wateja na dhima ya matini iliyokusudiwa kwa hadhira ya utamaduni lengwa (Vermeer, 1989).

Katika nadharia hii, tafsiri inatazamwa siyo tu kama mchakato wa uhawilishaji bali kama muundo mahususi wa tendo la kibinadamu, ambao ni sawa na matendo mengine yafanywayo na binadamu. Vermeer (1984: 101) kama alivyonukuliwa na Nord (1997: 29) anasema kuwa, kila matini huzalishwa kwa lengo fulani maalumu na lazima ikidhi lengo hilo. Kwa maana hiyo, lengo la tafsiri lazima lielezwe na liwekwe wazi kabla mfasiri hajaanza kutafsiri. Nadharia hii inasisitiza kuwa, kila tendo lina matokeo yake (Vermeer, 1989 na 2000; Reiss na Vermeer, 1994).

Vermeer (1989a) anaeleza kuwa, tafsiri huzalishwa kwa ajili ya hadhira mahususi, kwa lengo mahususi na katika muktadha maalumu. Nadharia hii inatathmini matini kwa kuzingatia malengo maalumu yanayowasilisha dhima iliyo sawa baina ya utamaduni chanzi na utamaduni lengwa. Kwa ujumla, nadharia hii imejikita katika malengo ya tafsiri ambayo huukilia mbinu na mikakati ya tafsiri inayotumika katika kutoa matokeo stahiki ya kidhima. Katika nadharia hii, Vermeer (1987a: 29) anazingatia zaidi mpokezi wa tafsiri kuliko chanzo cha matini kiasi kwamba anakielezea kitendo cha kutafsiri kama kuiwasilisha matini kwa muktadha lengwa, nia lengwa na hadhira lengwa katika mazingira lengwa. Kulingana na mkabala huu, tafsiri nzuri ni ile inayoruhusu hadhira lengwa kupata

tafsiri yenye ushikamani na matini chanzi (Nord, 1991a na 2003; Reiss na Vermeer, 1994; Vermeer, 2000; Lauscher, 2000). Aidha, nadharia hii inaakisi uhawilishaji wa jumla wa kiisimu wa nadharia ya maumbo na miundo ya sentensi ambayo kwa mujibu wa nadharia hiyo, mfasiri anapotafsiri anatakiwa kuhakikisha kuwa maumbo ya maneno na miundo ya sentensi za matini chanzi yanazingatiwa katika matini lengwa. Katika Nadharia ya *Skopos* suala la maumbo ya maneno na miundo ya sentensi hupuuzwa na mkazo huwekwa kwa mpokezi ama hadhira. Hii ina maana kuwa, nadharia hii inajali zaidi hadhira, na kwa mujibu wa nadharia hii lengo la kutafsiri matini mahususi linatakiwa lizingatie mahitaji ya hadhira lengwa. Kwa hiyo nadharia hii imejikita katika dhana ya tafsiri iliyojiegemeza zaidi kwenye dhima na utamaduni-jamii (Gentzler, 2001). Kwa ujumla, Nadharia ya Skopos imetusaidia kuchambua, kujadili na kutoa hitimisho la makala hii ambayo imelenga kutathmini mchango wa J.K. Nyerere katika maendeleo ya fasihi ya Kiswahili.

**Methodolojia**

Makala hii ililenga kufanya tathmini ya mchango wa tafsiri za J.K. Nyerere katika maendeleo ya fasihi ya Kiswahili. Ili kufikia lengo hilo, makala hii imetumia mifano kutoka katika matini chanzi na matini lengwa ya vitabu vya *The Merchant of Venice* "*Mabepari wa Venisi* na *Julius Caiser "Julius Kaizari"*. Mtafiti alitumia mbinu ya usomaji makini kwa kusoma kukusanya data za dondoo kutoka katika vitabu hivyo ambazo zimetumika kama mifano katika kujenga hoja na mjadala wa makala hii.

**Mchango wa Tafsiri za J.K. Nyerere katika Maendeleo ya Fasihi ya Kiswahili**

Kama tulivyoeleza hapo awali makala hii ililenga kujadili mchango wa tafsiri za J.K. Nyerere katika maendeleo ya fasihi ya Kiswahili. Katika makala hii tutajadili mchango huo kwa kuangazia pande mbili za kifani na kimaudhui. Kwa kuangazia mchango huo kifani na kimaudhui, tutaweza kuonesha jinsi tafsiri hizo zilivyochangia katika maendeleo ya fasihi ya Kiswahili. Tunatambua kwamba J.K. Nyerere amefanya kazi kubwa sana ya kutafsiri tamthiliya mbili za Shakespeare. Shakespeare ni mwandishi na mtunzi wa tamthiliya za The Merchant of Venice "*Mabepari wa Venisi* na Julius Caiser "Julius Kaizari". Mchango huo ni kama ifauatavyo:

**Mchango wa Kifani**

Kama tulivyoeleza tafsiri za J.K. Nyerere zina mchango mkubwa katika fani ya fasihi za Kiswahili. Kifani, tafsiri hizo zimechangia katika mtindo, mbinu za kifani, mbinu za utunzi na uandishi, ujenzi wa wahusika na lugha. Sehemu ifuatayo inajadili kwa kina kuhusu mchango wa tafsiri za J.K. Nyerere kifani.

**Mtindo**

Katika mtindo, mfasiri amezingatia mtindo wa kishairi katika utunzi wa tamthiliya ambao umetumiwa na mwandishi wa matini chanzi. Hivyo, uzingativu wa mtindo huu wa kishairi uliwapa athari na hamasa watunzi wa fasihi ya Kiswahili kutumia mtindo wa kishairi katika utunzi wa kazi zao za fasihi ya Kiswahili. Kwa mfano, mtindo wa kishairi tunauona katika baadhi ya tamthiliya za Kiswahili kama vile utunzi wa Ebrahim Husein (1971) katika tamthiliya yake ya *Mashetani* na Penina Mlama (1982) katika *Nguzo Mama* ametumia mtindo wa kishairi. Hivyo, tunaona kwamba kazi za tafsiri katika fasihi ya Kiswahili huweza kuibua mitindo mipya ya uandishi. Jamii huweza kutofautiana na huweza pia kuwa na mitindo mbalimbali ya utunzi na uandishi wa kifasihi. Hivyo, kazi ya fasihi inapotafsiriwa kutoka jamii moja kwenda nyingine, jamii lengwa hunufaika na mitindo ya uandishi iliyopo katika jamii chanzi. Katika tafsiri uzingalifu wa mitindo ni jambo la muhimu sana (Mwansoko na wenzake 2006).

**Kukuza na Kuendeleza Mbinu za Uandishi wa Kifasihi**

Tafsiri zilizofanywa na J.K. Nyerere zimekuwa ni chachu na hamasa ya kuendeleza uandishi wa kazi za fasihi ya Kiswahili hususani tamthiliya. Hii ni kutokana na watunzi wa tamthiliya kufahamu misingi na mbinu za uandishi na utunzi wa tamthiliya kupitia tafsiri za *Mabepari wa Venisi* na Julius Kaizari. Kwa mujibu wa Ruhumbika, (1978) anasema kuwa waandishi wengi wamejifunza mbinu za uandishi wa tamthiliya kutoka mataifa mengine. Mfano wa mbinu hizo ni kama vile mtindo, ujenzi wa wahusika na uundaji na ubunifu wa mandhari na mbinu nyinginezo za kisanaa.

**Mbinu za Utunzi**

Mbinu za utunzi wa kazi za fasihi huweza kuathiriana kutoka kwa mtunzi mmoja kwenda kwa mtunzi mwingine. Hii ni kutokana na kusoma kazi za mwandishi na hivyo kuathiriwa na kuiga utunzi wa mwandishi huyo. Kwa mfano, mtunzi Emmanuel Mbogo anasema;

> ''…Baada ya kuingia Chuo Kikuu cha Dar es Salaam utunzi na ufuasi wa Nadharia ya Umaksi uliniathiri hasa niliposoma tamthiliya za Bel Brecht na nadharia yake ya Kiepiki. Baadhi ya mbinu zake zinajitokeza katika tamthiliya yangu ya kwanza ya *Giza Limeingia*. Katika tamthiliya hiyo, nilifanya kitu kisicho cha kawaida ambacho kinaonesha mkengeuko, hasa pale nilipochanganya matendo ya jukwaani na matumizi ya filamu kwa wakati mmoja. Kwa mfano, tendo la kuwahamisha watu waende kwenye vijiji vya ujamaa. Sikatai kwamba utunzi wangu wa *Giza Limeingia* unaathari dhahiri za mbinu za Kiepiki za Bel Brecht.
>
> Kadri siku zilivyoendelea nilibadilika katika utunzi na ubunifu. Mimi ni mwandishi, si mwanasiasa wala mwanauchumi. Kila kazi ninayotunga lazima itoke kama sanaa katika lugha na muundo wa kazi na mbinu za kisanii kama mwandishi nizijue na niandike kama mbunifu kwa sababu niliona kwamba, masuala ya kisiasa na itikadi za kimaksi nikiziingiza sana katika uunzi nitaishia kuuwa ubora wa ujumi wa kazi ya sanaa. Baada ya kujua hilo nikaanza kukazania kusoma tamthiliya za Shakespeare *Julius Kaizari*, "*Macbeth*" na *Mabepari wa Venisi* (1969). Vilevile nilisoma tamthiliya ya "*Mfalme Edipode* (1971)". Ilikuwa kazi ngumu sana kusoma na kuzielewa hasa tamthiliya za Shakespeare zilizokuwa zimeandikwa lugha ya Kiingereza. Aidha nakiri kwamba, tafsiri hasa ya Nyerere na Mushi kazi hizo ilinipa mwanga na uelewa zaidi katika kutunga tamthiliya zenye ujumi uliokomaa. Kwa maana hiyo, utunzi wangu wa tamthiliya ya *Morani* (1993) ndiyo niliyoanza kuzingatia usanii na usanaji wa lugha ya kisanii ya kiwango cha juu. Kwa mfano, matumizi ya sitiari, jazanda, kejeli, tashititi, muundo n.k. katika kuelezea uhalisia wa maisha ya jamii. Wakati huohuo nilizisoma tamthiliya ya Wolesoyinka tena na tena na tena…'' Jilala (2016).

Ukichunguza maelezo ya Emmanuel Mbogo yanathibitisha kuwa utunzi wake wa tamthiliya, mbinu na matumizi ya sitiari, jazanda, kejeleli, tashtiti, muundo n.k ni matokeo ya athari aliyoipata kwa kusoma vitabu vya tamthiliya za Shakespeare zikiwemo zile zilivotafsiriwa na J.K. Nyerere vya *Mabepari wa Venis* na. Aidha, anathibitisha kuwa ilikuwa kazi ngumu kusoma na kuelewa vitabu hivyo bali tafsiri ya *Julius Kaizari* vitabu hivyo zilizofanywa na J.K. Nyerere zilimpa mwanga na uelewa zaidi katika kutunga tamthiliya zenye ujumi uliokomaa. Kupitia maelezo hayo tunaweza kusema tafsiri za J.K. Nyerere zimechangia katika maendeleo ya fasihi ya Kiswahili. Hii ina maana kuwa wapo wasanii ambao utunzi wa tamthiliya zao umetokana na kusoma kazi za tafsiri za tamthiliya za Shakespeare ambazo zimeimarisha stadi na maarifa ya utunzi, matumizi ya lugha, mbinu za utunzi, uteuzi wa msamiati, uumbaji wa wahusika, muundo na mtindo wa kazi za fasihi ya Kiswahili.

**Mbinu za Tafsiri**

Mbali ya mchango wa kifani na kimaudhui, J.K. Nyerere ametoa mchango mkubwa katika mbinu za tafsiri ya matini za kifasihi. Katika tafsiri yake ametumia mbinu ya kisemantiki na kimawasiliano ili kukidhi mahitaji ya hadhira lengwa, utamaduni na mazingira ya hadhira aliyoikusudia. Hivyo, mchango wake katika mbinu za tafsiri umesaidia kusukuma mbele ari na moyo wa wafasiri wengine kupata ujasiri na uwezo wa kufasiri matini za lugha nyingine kwenda katika lugha ya Kiswahili. Hii

imechangia kutoa mwanya na fursa ya matini nyingi za fasihi kutafsiriwa katika Kiswahili. Mfano, ni tafsiri ya *Song of Lawino* iliyofanywa na Paul Sozigwa kama *Wimbo wa Lawino*. Mwansoko (2001) anasema Paul Sozigwa alifanya kazi kwa karibu sana na J.K. Nyerere. Hivyo, hapana shaka kuwa alihamasishwa na kutiwa moyo na tafsiri za J.K. Nyerere na kuona kuwa yeye pia anaweza kutafsiri *Song of Lawino*.

**Ukuzaji wa Lugha ya Kiswahili Duniani**

Lugha ndiyo chombo na nyenzo muhimu katika fasihi yoyote duniani. Lugha hutumika kuwasilishia fasihi ya lugha husika. Hivyo, tafsiri ya J.K. Nyerere imesaidia kukitangaza Kiswahili kimataifa na kuifanya kuwa ni lugha ambayo inatazamwa kwa jicho la kitafiti. Aidha, watu wengi duniani wamekuwa na hamasa ya kutaka kujifunza lugha ya Kiswahili kutokana na kuiona ikitumika katika kutafsiri fasihi ya lugha zao. Mwansoko (2016) anasema tunapoona kazi za tafsiri katika Kiswahili kutoka Kiingereza, Kichina, Kikorea, Kirusi, Kifaransa, na kadhalika, maana yake ni kuwa Kiswahili kimetambulishwa pia katika jamii za kigeni zinazotumia lugha hizo. Mfano halisi ni uthubutu wa Baba wa Taifa la Tanzania, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, wa kutafsiri katika Kiswahili tamthiliya mbili za mwandishi mashuhuri wa Uingereza wa karne ya 16, William Shakespeare. Tamthiliya hizo ni *Julius Caesar* (ambayo ni tanzia) na *The Merchants of Venice* (ambayo ni futuhi au ramsa). Kwamba ziliweza kufasirika katika Kiswahili kuwa *Juliasi Kaizari* (1963) na *Mabepari wa Venisi* (1969) mtawalia ni uthibitisho kuwa lugha ya Kiswahili ni pevu vya kutosha kuweza kueleza dhana anuwai na utamaduni uliokuwa umebebwa katika maandiko hayo ya Kiingereza cha kale. Kwa hakika lilikuwa ni tukio la mshangao kwa Waingereza na Wazungu wengine duniani kusikia kuwa William Shakespeare ameweza kutafsirika kwa lugha ya Kiafrika iitwayo Kiswahili. Na jambo hili yawezekana ndilo limekuwa kichocheo cha Wazungu kutaka kuifuatilia lugha hii kiutafiti na kujifunza pia ili nao waizungumze. Huu ni uthibitisho kuwa tafsiri imekitangaza Kiswahili ulimwenguni.

**Kukuza Msamiati na Istilahi za Kiswahili**

Kazi yoyote ya fasihi hutegemea msamiati katika kuwasilisha ujumbe wake. Tafsiri ya vitabu vya Shakespeare zilizofanywa na Mwalimu Nyerere zimechangia katika ukuzaji wa msamiati wa Kiswahili ambao pia ni utajiri katika kuendeleza fasihi ya Kiswahili. Tamthiliya zilizotafsiriwa zimesaidia kuibua na kuongeza msamiati wa lugha ya Kiswahili. Ongezeko hili la msamiati mpya linasaidia jamii ya Kiswahili kufahamu na kutumia maneno mapya katika kurejelea dhana tofauti tofauti kulingana na muktadha wa matumizi yake. Mwansoko (2016) anasema Mwalimu Nyerere katika tafsiri amechangia ukuzaji wa msamiati na istilahi za Kiswahili kupitia mbinu mbili; mbinu ya ukopaji na mbinu ya kubuni istilahi. Kwa mfano, Mwalimu Nyerere alisaidia kukopa misamiati mipya kama vile:

i. Filosofa-philosopher (msamiati sanifu wa sasa ni ‘mwanafalsafa’).
ii. Stokingi-round hose (Kamusi ya Johnson (1939) imefasili dhana hii kuwa ‘stoki’. Sasa hivi ‘stokingi’ ni sanifu).
iii. Paithagorasi - Pythagoras
iv. Frankifuti - Frankfurt
v. Tripoli - Tripolis
vi. Liziboni - Lisbon.

Vilevile, kupitia mbinu ya kubuni ama kuunda msamiati mpya yeye mwenyewe. Mifano ifuatayo inadhihirisha hilo

i. Mlinzi - jela- gaoler (msamiati sanifu sasa ni ‘askari jela’/’mlinzi wa gereza’, ‘magereza’). Wakuu watatu waliotawala kwa shirika baada ya kifo cha Juliasi
ii. Kaizari-triumvirs (msamiati sanifu sasa ni ‘utawala wa watu watatu’).

**Chanzo:** Julius Kaizari

**Uingizaji wa Miundo Mipya ya Misemo katika Kiswahili**

Miongoni mwa mbinu za tafsiri, ambazo Mwl. J.K. Nyerere amezitumia katika kutafsiri tamthiliya za Shakespeare ni tafsiri ya kisemantiki (au tafsiri ya wazi). Mbinu hii imechangia kwa kiwango kikubwa kuingiza miundo mipya ya misemo katika lugha ya Kiswahili kutoka kwenye lugha ya Kiingereza. Kwa ujumla, tafsiri ya kisemantiki huegemea zaidi upande wa mwandishi wa matini chanzi na kutaka kufasiri kila kipashio katika matini hiyo. Kila dhana katika LC huelezwa kwa neno mahususi katika LL, jambo ambalo huifanya tafsiri ya kisemantiki ionekane kuwa ni tafsiri fafanuzi. Hivyo, uingizaji wa miundo mipya na misemo katika lugha ya Kiswahili inasaidia katika kukuza fasihi ya Kiswahili. Tazama mifano hapa chini:

> *Ant*. In sooth, I know not why I am so sad.
> It wearies me; you say it wearies you;
> But how I caught it, found it, or came by it,
> What stuff 'tis made of, whereof it is born,
> I am to learn;
> And such a want-wit sadness make of me
> That I have much ado to know myself.
>
> ANTONIO: Kusema kweli sijui kisa cha huzuni yangu;
> Inanitabisha sana; wasema yakutabisha;
> Bali nilivyoipata, au kuiambukizwa,
> Au imejengekaje, imezawa jinsi gani,
> Ningali sijafahamu,
> Na huzuni yanifanya kuwa kama punguani,
> Kunifanya nisiweze kujifahamu mwenyewe.
>
> *Chanzo*: Mabepari wa Venisi

Ukichunguza mfano hapo juu utaona kuwa ujumbe wa matini chanzi umemlazimu mfasiri kutumia tafsiri ya kisemantiki na hatimaye kuunda miundo na misemo mipya. Kama ambavyo nadharia ya Scopas inasema lengo la tafsiri huukilia njia ili kueleta maana na ujumbe wa matini lengwa. Kwa mfano matumizi ya maneno; 'inanitabisha' ambapo angeweza kusema 'inanipa taabu, inanitesa ama inanisumbua', 'yakutabisha' ingeweza kuwa inakupa taabu, inakusumbua ama inakutesa', 'kuiambukizwa' ingeweza kuwa nilivyoambukizwa huzuni, 'imejengekaje' ingeweza kuwa imetengenzwa vipi, 'imezawa' ingeweza kuwa imezaliwa, 'sijifahamu' ingeweza kuwa sijitambui, sijielewi, 'kujifahamu' ingeweza kuwa kujitambua, kujielewa na neno 'kisa' ingeweza kuwa chanzo ama sababu.

**Kukuza Fasihi ya Kiswahili**

Tafsiri za maandiko ya kifasihi kutoka lugha zilizoendelea, hasa za waandishi mashuhuri, hupanua kiwango cha fasihi ya Kiswahili, kwa sababu maandiko hayo aghalabu huwakilisha matokeo ya urithi wa vizazi na vizazi, na mara nyingine hata kwa zaidi ya karne. Utajiri wa fasihi hizo huchangia katika makuzi ya fasihi ya Kiswahili. Kwa mujibu wa Ruhumbika (1978) anasema kuwa waandishi wengi wamejifunza mbinu za uandishi wa tamthiliya kutoka mataifa mengine. Mfano wa mbinu hizo ni kama vile mtindo, ujenzi wa wahusika na uundaji na ubunifu wa mandhari na mbinu nyinginezo za kisanaa. Mbinu hii ya tafsiri imefanya fasihi ya Kiswahili kukua na kuweza kuendelea kufanyiwa ulinganisho na fasihi nyingine za ulimwengu, mfano: tamthiliya ya "*Amezidi"* ya Said A. Mohamed. Mfano wa kazi zilizotafsiriwa; *Aliyeonja Pepo*, *Nitaolewa Nikipenda* yake Ngugi wa Thiong'o, *Adui wa Umma* na *Orodha.* Vilevile, tafsiri imesaidia kuendeleza fasihi ya Kiswahili na utamaduni wake katika jamii tofautitofauti kwa mfano, kuna kazi za fasihi ya Kiswahili zikiwemo tamthiliya za Kiswahili zilizotafsiriwa ambazo ni pamoja na; *Tufani* ya Samweli S. Mushi, *Shetani Msalabani*, *Mtawa Mweusi* na *Nitaolewa Nikipenda* zake Ngugi wa Thiong'o.

**Kuongeza Idadi ya Machapisho**

Tafsiri ya J.K. Nyerere imesaidia kuongeza machapisho ya kazi za fasihi hususan tamthiliya. Tamthiliya hizi ambazo zilifanywa na J.K. Nyerere zinasomwa kama kazi za fasihi ya Kiswahili na hivyo kuongeza idadi ya vitabu vya tamthilliya katika Kiswahili. Faida nyingine tunazoweza kuziongezea hapa ni pamoja na kutia shime na kuendeleza uandishi wa kifasihi, kupanua hadhira ya kazi ya fasihi, kuongeza msamiati wa lugha na kadhalika. Kabla ya kuzama sana na kuweza kubainisha na kuchambua kazi za tafsiri katika tamthiliya ya Kiswahili ni vema kwanza tufafanue kwa kina dhima hizi za tafsiri.

**Kutajirisha Fasihi ya Kiswahili**

Kupitia tafsiri ya vitabu vya Shakespeare ziliziofanywa na Mwalimu J.K. Nyerere tunaoana kuwa zimesaidia kutajirisha fasihi ya Kiswahili. Ni dhahiri kwamba uwepo wa vitabu hivyo katika lugha ya Kiswahili vimesaidia kutajirisha fasihi ya Kiswahili na kuongeza idadi ya matini za kifasihi katika lugha ya Kiswahili ambazo zinatumiwa katika kufundisha na kujifunza fasihi ya Kiswahili. Pia, tafsiri inakuza lugha ya fasihi husika, kupitia tafsiri msamiati mpya unaingia katika lugha husika tukijua kuwa lugha ndio mhimili wa fasihi, kwa hiyo msamiati ukiimarika fasihi pia huimarika. 'Lugha nyingi za Kiafrika, Kiswahili kikiwa miongoni mwao, hazikuwa zimeendelea sana kimaandishi hasa maandishi ya kufasiri kwa hiyo tafsiri za tamthiliya zikilenga kukuza maandishi ya lugha za Kiswahili. Na vilevile tamthiliya ilitafsiriwa kwa lengo la kuongeza machapisho ya fasihi ya Kiswahili'' (Ruhumbika, 1978). Kwa mujibu wa Mwansoko (1996) anasema shughuli za wazalendo zimejadiliwa na mashirika ya utafsiri na uchapishaji ya nchi za nje ambayo yamefanya kazi kubwa ya kupanua hazina ya vitabu vya Kiswahili. Baadhi ya mashirika hayo ni; Shirika la Uchapaji Lugha za Kigeni, Beijing, China, miongoni mwa tafsiri za Kiswahili za mashirika haya ni pamoja na *Shajara ya Mwenda Wazimu* na *Hadithi Teule*. Kutokana na maendeleo ya tafsiri fasihi ya Kiswahili imesambaa na kuwafikia watu wa mataifa mbalimbali.

**Mchango wa Kimaudhui**

Tafsiri zilizofanywa na Mwl. J.K. Nyerere zimetoa mchango mkubwa katika maendeleo ya maudhui ya kazi za fasihi ya Kiswahili. Hii ni pamoja na watunzi kupata na kufahamu mbinu za kutumia Sanaa ya tamthiliya kuibua na kuelezea matatizo ya jamii, kuonya, kuelimisha na kurithisha amali za jamii. Hivyo, tunaweza kusema kwamba tafsiri za J.K. Nyerere zimesaidia katika kuibua maendeleo ya dhamira, falsafa, migogoro na utatuzi wa migogoro na suluhisho la migogoro katika jamii lengwa. Kwa kusoma na kufahamu falsafa ya mtunzi, visa na matukio, migogoro na namna ya kutatua migogoro na kuelezea dhamira hizo ndani ya jamii imesaidia kuwapa maarifa watunzi wa fasihi ya Kiswahili kuweza kufahamu namna ya kutumia fasihi kujadili dhamira mbalimbali ndani ya jamii.

Hivyo, tafsiri imeweza kuibua aina mpya ya maudhui. Hii ina maana kuwa kazi inapotafsiriwa kutoka jamii lugha ambayo imepiga hatua kubwa kimaendeleo kunakuwa na maudhui mapya ambayo yanaweza kuingizwa katika fasihi lengwa hivyo kuweza kuamsha ari ya kimapinduzi. Kwa mfano, inapotokea jamii yenye ukandamizaji wa wanawake ila haina mwamko wa kupinga ukandamizaji huo wa wanawake, jamii lengwa huweza kupata mwamko na kujifunza kwamba kukomeshwa kwa ukandamizwaji wa wanawake ni jambo linalowezekana.

Tafsiri za Shakespeare zilizofanywa na J.K. Nyerere zimechangia katika maudhui ya fasihi ya Kiswahili. Maudhui ya tamthiliya za Shakespeare yana umuhimu mkubwa kwa taifa changa kama Tanzania. Tamthiliya za *Julius Kaizari* na *Mabepari wa Venis* zinaonesha na kulaani kwa uwezo mkubwa wa kisanii udhalimu na madhambi ya mfumo wa kinyanyasaji na unyonyaji wa kibepari. Jamii za kibepari zimeonyesha jinsi zinavyoabudu utajiri, zinavyopenda makuu, vyeo na utawala wa kidikteta na jinsi zisivyojali utu na haki za binadamu. Mwalimu Nyerere akiwa amedhamiria kujenga taifa la kidemokrasia na lenye kufuata itikadi ya ujamaa inayotoa fursa sawa kwa wananchi wake wote, alitafsiri tamthiliya hizi na kuonesha hisia zake za kukerwa na itikadi ya ubepari, kuibua mtazamo huohuo hasi dhidi ya ubepari miongoni mwa wasomaji wa tafsiri zake.

**Uibuaji na Maendeleo ya Dhamira**

Kupitia tafsiri za J.K. Nyerere, tunaona kuwa mfasiri amechangia katika uibuaji na kusaidia maendeleo ya dhamira za kazi za fasihi. Kwa mfano, mtunzi wa matini chanzi ametumia sanaa kuibua dhamira mbalimbali ndani ya jamii kama vile uongozi mbaya, haki na sheria, mapenzi, nafasi ya mwanamke, matabaka, ubepari na athari zake. Kupitia tafsiri, ni dhahiri kuwa watunzi wa fasihi ya Kiswahili wamejifunza, kuathiriwa na kuiga mbinu za kisanaa katika kuelezea na kuibua masuala ya kijamii. Mfano, kufahamu kuhusu dhamira ya matabaka yaliyopo katika matini zilizotafsiriwa imesaidia kuelewa dhamira hizo na jinsi zinavyofafanana katika jamii lengwa. Kwa mfano, kupitia tafsiri hizo tumeweza kuona dhamira ya ubepari na ubwenyenye na athari zake katika jamii. Kutafsiri *Merchant of Venice* kama *Mabepari wa Venisi* imefanywa kwa makusudi kwa lengo la kuonesha athari za ubepari katika ujenzi wa jamii mpya. Ikumbukwe tafsiri hizi zilifanyika miaka michache baada ya uhuru wa Tanganyika ambapo jitihada za nchi zilikuwa ni kujenga jamii mpya yenye mrengo wa falsafa ya ujamaa na kujitegemea huku ikipinga ubepari, unyonyaji, ukandamizaji na kujilimbikizia mali. Aidha, mfasiri ameibua dhamira kama vile ubepari, unyonyaji, utawala wa kidikteta, mapenzi, haki na sheria. Dhamira ambazo waandishi wa fasihi ya Kiswahili wameendelea kutumia mbinu za kisanii kuziibua na kuzidhihirisha ndani ya jamii kwa kutumia kalamu zao.

**Falsafa na Itikadi**

Kupitia tafsiri hizi tunaona jinsi mfasiri J.K. Nyerere alivyoibua falsafa na itikadi ya ujamaa kwa kuonesha uovu wa ubepari, unyonyaji na ubwanyenye na athari zake katika jamii. Hii imejidhihirisha kwa kutafsiri *Merchant of Venice* kama *Mabepari wa Venisi* inaonesha dhahiri jinsi mfasiri alivyokuwa na falsafa na itikadi tofauti na misingi ya ubepari. Hivyo, kwa kusoma kazi hizi zilizotafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili, hadhira lengwa wameweza kuona jinsi maendeleo ya falsafa na itikadi ya ujamaa na kujitegemea inavyowasilishwa na mfasiri kupitia tafsiri yake. Aidha, uteuzi wa msamiati unajiegemeza katika imani, itikadi na falsafa ya mfasiri. Kwa mfano uteuzi wa neno "mabepari" badala ya "wafanya biashara" inadhihirisha imani, falsafa na itikadi ya mfasiri.

**Kuibua Tamaduni za Jamii**

Tafsiri iliyofanywa na J.K. Nyerere imesaidia kuibua tamaduni za jamii asilia ya fasihi chanzi kwa jamii lengwa. Kuifanya jamii lengwa iweze kuufahamu utamaduni na fasihi ya jamii chanzi kupitia tafsiri ya Kiswahili. Aidha, jamii lengwa inaweza kujifunza, kuiga na kulinganisha utamaduni chanzi na utamaduni lengwa. Hivyo, kupitia tafsiri zilizofanywa na J.K. Nyerere ni rahisi pia kujifunza na kulinganisha tamaduni, mila, desturi na kaida za jamii chanzi na kuzihamishia katika jamii lengwa. Tafsiri hizo zimesaidia kutambulisha kwa hadhira wa fasihi ya Kiswahili utamaduni wa kimwinyi na kibwanyenye uliopo katika nchi za Ulaya Magharibi.

**Kuongezeka kwa Hadhira**

Tafsiri ya tamthiliya za Shakespeare zilizofanywa na J.K. Nyerere zimesaidia kuongeza hadhira ya wasomaji wa matini hizo. Wasomaji na wachambuzi wa fasihi ya Kiswahili ambao huweza kusoma, kuhakiki na kujadili matini hizo kama kazi za fasihi ya Kiswahili.

**Hitimisho**

Makala hii imetathmini mchango wa tafsiri za J.K. Nyerere katika Maendeleo ya Kiswahili. Katika Makala hii tumejadili kuwa tafsiri zilizofanywa na J.K. Nyerere ni hazina kubwa katika maendeleo ya fasihi ya Kiswahili na hususan katika ujenzi wa fani na maudhui ya kazi za fasihi. Kupitia tafsiri hizo watunzi wa tamthiliya wameweza kujifunza mbinu za ubunifu, kanuni na taratibu za utunzi wa tamthiliya na namna ya kujenga, kusuka na kuendeleza visa na matukio katika matini za kifasihi. Aidha, makala hii imejadili kuwa tafsiri za J.K. Nyerere zimechangia katika kukuza na kuimarisha stadi za utunzi, mtindo na maendeleo ya dhamira, kukuza na kutangaza lugha ya Kiswahili duniani, kutajirisha machapisho ya Kiswahili na kukuza msamiati wa lugha ya Kiswahili. Kwa ujumla, dunia imeweza kuwasiliana na kutangamana kupitia tafsiri ambayo imetumika kama nyenzo na daraja muhimu la kuwaunganisha watu wa jamii, lugha na tamaduni tofauti na kuwafanya waweze

kuwasiliana na kuelewana, kupata maarifa, uzoefu, mila na desturi zilizofungamana na utamaduni huo. Hivyo, tafsiri ya J. K. Nyerere zilikuwa ni dira na mwanga uliomulika na kuchochea harakati zingine za kutafsiri matini za kifasihi kutoka lugha zingine kwenda Kiswahili na kinyume chake.

**Marejeo**

Catford J.C. (1965). *A linguistic translation theory of*: An easy in Applied Linguistics. London: Oxford press.

Baker, M. na Saldanha, G. (2009). *Routledge Encyclopedia of Translation Studies*. Newyork: Routledge.

Jilala, H. (2016). Misingi ya Fasihi Linganishi: Nadharia, Mbinu na Matumizi. Dar es salaam. Daud Publishin Company Ltd.

______(2014). Athari za Kiutamaduni katika Tafsiri: Mifano kutoka Matini za Kitalii katika Makumbusho za Tanzania. Tasnifu ya Uzamivu (Ph.D Kiswahili) (haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

_____(2014b). Matatizo ya Tafsiri katika Matini za Kitalii Nchini Tanzania in *Kioo cha Lugha*

Jarida la Taasisi ya Taauma za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Juzuu Na. 12 uk.na. 27- 47.

Katan, D. (1999). *Translating Culture: An Introduction for Translators, Interpreters and Mediators.* Manchester: St. Jerome Publishing.

Klaudy, K. (2003). *Languages in Translation Lectures on Theory, Teaching and Practice of Translation*. Budapest: Scholastica.

Koller, W (1990). The Concept of Equivalent and The Object of Translation Studies. *Target, 2*, uk. 191-222.

Lauscher, S. (2000). Translation Quality Assessment: Where can Theory and Practice Meet? *The Translator,* Juzuu Na. 6, (2), kur.149-168.

Lin, X (2006). Employment of The Functional Concept in The Chines-English Translation of Tourist Material.In *Journal of Fujian Normal University*. Juzuu Na. 2. Uk. 135-140.

Malangwa, S. P (2005). Problems of Translating Literary Works: The Case of Julius Kambarage Nyerere's Translation of The Play Mabepari wa Venisi. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

________(2010). "Handling Technical Translations: The Case of Translation of Computer Programs from English into Kiswahili." Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Maltin de Leon, C. (2008). *Skopos and Beyond.* Amsterdam: John Benjamins Publishing Company.

Meschonnic, H. (2003).Texts on Translation. Katika A. Pym (Mh.), *Introduction and Translation.* Target, Juzuu Na.15: 2, kur. 337-353.

Method, S. (2015). *Umahiri katika fasihi ya Kiswahi*: Mwongozo kwa mwanafunzi na mwalimu wa fasihi simulizi na andishi. Dar es Salaam: Meveli Publishers (MVP).

Micaela, M. (2008). *An Approach to New Trends in Translation and Culture Identity.* Newcastle Upon Tyne, NE6 2XX, UK: Cambridge Scholars Publishing 12 Back Chapman Street.

Munday, J. (2001). *Introducing Translation Studies. Theories and Application*. London: Routledge.

Mutasa, V. E (1999). Problems of Translation of Newspaper Articles. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mwansoko, H. J. M. (1996). *Kitangulizi cha Tafsiri: Nadharia na Mbinu*. Dar es Salaam: TUKI

Mtui, J. A (2009). The Adequacy of Translation Theory with Respect to Drama: The Case of Samwel Mushi's Mfalme Edipode. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Munday, J. (2012). *Introducing translation studies: Theories and applications*, Tol. 3, London na New York: Routledge-Taylor & Francis Group.

Newmark, P. (1981). *Approaches to translation*, Oxford na New York: Pergamon.

Newmark, P. (1988). A *Textbook of Translation*. London: Prentince Hall.

Nida, E. A. (1975). *Componential Analysis of Meaning. An Introduction to Semantic Structures.* Paris: Mouton.

_______ (1964). *Towards a science of Translating*. Leiden: EJ. Brill.

_______ (2001). Language *and Culture: Context in Translating*. Shanghai: Shanghai Foreign Language Ed Press.

Nida, E. A. na Taber, C. (1969). *Theory and Practice of Translating*. Leiden: Brill.

Nord, C. (2001). *Translating as A Purposeful Activity: Functionalist Approaches Explained*. Manchester: St. Jerome Publishing.

Nord, C. (1991a). Skopos, Loyalty and Translational Conventions. *Target,* 3 (1), uk. 91-109.

_______ (1997). *Translating as A Purposeful Activity: Functionalist Approaches Explained*. Manchester: St. Jerome.

________ (2001). *Translating as A Purposeful Activity: Functionalist Approaches Explained*. Manchester: St. Jerome Publishing.

_______ (2005). *Text Analysis in Translation: Theory, Methodology and Didactic Application of A Model for Translation-Oriented Text Analysis* (toleo la 2). New Jersey: Rodopi B.V. Amsterdam-New York.

Nyerere, J.K. (1969). *Mabepari wa Venisi*: Tafsiri ya Merchant of Venice ya William Shakespeare. Oxford University Press: Nairobi.

Reiss, K. na Vermeer, H (1994). *Groundwork for a General Theory of Translation*. Tubingen: Niemeyer.

Ruhumbika, G. (1983a). Tafsiri za Maandishi ya Kigeni katika Kiswahili katika Makala za Semina ya Kiamtaifa ya Waandishi wa Kiswahili 11, Uandishi na Uchapishaji, Dar es salaam, TUKI: 83 – 97.

_________ (1983b). *Tafsiri za Fasihi za Kigeni katika Ukuzaji wa Fasihi ya Kiswahili*. Makala katika Makala za Semina ya Kimataifa ya waandishi wa Kiswahili 111, Fasihi, Dar es salaam, TUKI. uk. 253-266.

Schäffner, C (1998). Skopos Theory. Katika M. Baker (Mh.) *Routledge Encyclopedia of Translational Studies*. London: Routledge. uk. 235-238.

Shakespeare, W. (1987). *The Merchants of Venice* by M.M. Mahood (Ed). Cambridge: Cambridge University Press.

Shen, J (2005). Skopos Theory and The Trategy for C-E Advertising Discourse Transaltion. In *Journal of Zhejiang*: Normal University. Toleo la 2, Uk. 69-74

Stajszczak, T (2011). *Skopos Theory as An Aid in Resolving Culture-Related Difficulties in The Translation of Functional Texts*. Warsaw: University of Warsaw.

Su-zhen, J (2008). *Skopos Theory and Translating Strategies of Cultural Elements in Tourism Texts*. Iliyopakuliwa Julai, 21, 2010, katika http://www.linguisti.org.n/doc/su20080906.pdf.

Vermeer, H. (1989). Skopos and Commission in Translational Activity. Katika Venuti, L. (Mh.). *The Translation Studies Reader*. London: Routledge.

_________ (1987). What does It mean to Translate? Katika *Indian Journal of Applied Linguistic* Juzuu Na. 13 (2), kur. 25-33.

________ (1989a). Skopos and Commission in Translational Action. Katika A. Chesterman (Mh.). *Readings in Translation Theory*. kur. 99-104.

_________ (1989). Skopos and Commission in Translation Action. Katika A. Chesterman (mh.). *Readings in Translation Theory*. Oy Finn Lectura Ab, kur.173-187.

_________ (1999). *A Skopos Theory of Translation*. Heidelberg: Textcon Text.

_________ (2000). Skopos and Commission in Translation Action. Katika L. Venuti, (Mh.), *The Translation Studies Reader*. New York: Routledge, uk. 227-237.

Venuti, L (2002). *On The Different Methods of Translating*. The Translation Studies reader.

Wafula, R.M (1999). *Uhakiki wa tamtiliya*, *Historia na maendeleo yake*. Nairobi Kenya: Jomo Kenyatta Foundation.

Zhang, J (2004). "Skopos Theory and Translation Methods in Chines Science and Technology. *Translators Journal*. Toleo la 1. uk. 35-37.